# UONGOZI NA STADI ZAKE

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **LG:** | (Lumen Gentium) Fumbo la Kanisa |
| **AA** | (Apostatian Actuostatem) Utume wa Walei |
| **TEC** | (Tanzania Episcopal Conference) Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania |
| **AMECEA** | (Association of Member Episcopal Conference of Eastern: Africa) Baraza la Maaskofu Katoliki Afrika Mashariki na Kati. |

Kitabu hiki kimeandikwa na:-
Bw. Augustine Nyange
Jimbo Katoliki la Moshi
MOSHI

Toleo la Kwanza - Feb. 2012

**Kimepigwa chapa na:-**
**HUBERT Company**
**Printing Works & General Services**
**P.O.Box 13428**
**Dar es Salaam**

# YALIYOMO

Dibaji .................... iii
Shukrani .................... iv
Utangulizi .................... v
Kanisa .................... 1
Mtaguso Mkuu II Vatikani
Hati ya Walei .................... 4
Walei na Uongozi Ndani ya Kanisa .................... 8
Kamati ndogo ndogo za Halmashauri Walei .................... 23
Mikutano .................... 29
Hitimisho .................... 32

# DIBAJI

Kitabu hiki kidogo kinahusu wewe mlei mbatizwa. Kwa ubatizo umeshirikishwa kikamilifu ukuhani, uongozi na unabii (ualimu) wa Yesu Kristu. Umeitwa kuwa mtu mwajibikaji ndani na nje ya kanisa.

Kitabu hiki kinakusudiwa kwa ajili yako wewe Mkristu unayeishi hapa Tanzania na kwa namna ya pekee hapa jimbo Katoliki la Moshi. Kimeandikwa kwa ajili yako, kikusaidie kujua na kuelewa maana ya Uongozi Bora na hivyo kushiriki kikamilifu katika utume wa Kanisa Mahalia.

Wakati huo huo kitabu kimeandaliwa mahususi kwa ajili ya:

- Kiongozi mlei wa Halmashauri ya Walei, Chama cha Kitume au jumuiya ya Kitume afahamu barabara dhamana ya uongozi, haki na wajibu wa kiongozi.

- Katekista au mwalimu wa dini shuleni

- Kila mkristo anayetamani kukua katika utume, kujua mambo ya msingi ya Uongozi bora na utume wa kanisa.

Tunalo tumaini kwamba kitabu hiki kitaeleweka na kuwasaidia wengi. Msomoji apate furaha ya kufahamu Uongozi bora na autekeleze.

Msgr. Paul Uria
Mshauri Kazi za kitume
Jimbo Katoliki Moshi

# SHUKRANI

Napenda kumshukuru Mungu kwa uhai anaotujalia siku hadi siku ili tutekeleze wajibu alizotupa kama Walei washiriki wa utume wa kanisa uletao wokovu

Namshukuru sana Msgr. Paul Uria kwa kunipa moyo wa kuandika kitabu hiki cha Uongozi na Stadi zake ili niwashirikishe Walei wenzangu mang'amuzi niliyo nayo katika uongozi na Stadi zake.

Namshukuru Mwenyekiti wa Halmashauri Walei jimbo Katoliki Moshi Baba Gaspar Makiluli kwa kunitia moyo nilipoanza kazi ya uandishi wa kitabu hiki, akitoa mawazo yake na uelewa wake kufikia mambo yatakayokidhi hitaji la Uongozi Walei Jimboni na popote watakapokitumia.

Nawashukuru wachapaji wa kitabu hiki kwa moyo wao wa uvumilivu pale nilipowarudiarudia kuongeza au kupunguza neno la uandishi.

Kwa ujumla nawashukuru wote walionisaidia kwa njia moja au nyingine kukiwezesha kitabu hiki kuwa kama kilivyo.

*"ASANTENI SANA MUNGU AWABARIKI"*

# UTANGULIZI

Baada ya kuwa katika Uongozi wa Shirika la Moyo Mtakatifu wa Yesu ngazi mbalimbali Parokia, Jimbo na Taifa kwa vipindi mbalimbali nimeshawishika niwashirikishe Walei wenzangu suala la Utume wa Kanisa na wajibu zetu katika kanisa.

Katika kitabu hiki nitaelezea kwa ufupi mambo yatakayokidhi hitaji letu kama Viongozi wa Kanisa Walei

**I. Kanisa ni nini?**

**II. Walei katika Kanisa**

**III. Walei na Uongozi ndani ya Kanisa**

- (a) Uongozi ni nini
- (b) Uongozi katika Kanisa
- (c) Sifa za Uongozi
    - i. Sifa za kiroho
    - ii. Sifa za kiutendaji
- (d) Wajibu wa jumla za Kiongozi katika kanisa
- (e) Majaribu Katika Uongozi

**IV. Mikutano na taratibu za mikutano ya Halmashauri Walei, Vyama/Mashirika na Jumuiya za Kitume**

Uongozi bora unapokuwepo kunaleta mafanikio lakini Unapokosekana kunarudisha nyuma maendeleo ya Kanisa na ya jamii nzima ya wanadamu.

Kwa kutumia kitabu hiki Walei watajifunza na kuelewa ili waamue kujirekebisha pale walipokuwa wakifanya tofauti na mwongozo wa Mapapa, Maaskofu na Mapadre wetu.

**Tumsifu Yesu Kristu.**

# SURA YA KWANZA

## KANISA

Tunapotaka kuangalia ya Walei katika Kanisa na Uongozi wa Walei katika Kanisa yatupasa kujua kwanza Kanisa

### 1. KANISA NI NINI?

**1.1** (a) Kanisa ni "Zizi" ambamo Kristo ndiyo mlango yeye asema:- "*Mimi ni mlango wa kondoo, anayeingia kwa kupitia kwangu ataokolewa" (Yoh. 10:7 - 9)*

Katika Zizi hilo ndiko wanakusanyika kondoo ambao Mungu ni mchungaji wake. Yeye asema "*Mimi mwenyewe nitawatafuta kondoo wangu (wanadamu) na kuwatunza, nitawakusanya kutoka nchi za mbali na kuwaleta katika nchi yao wenyewe, nitawapa malisho mazuri, wanaotangatanga kwa kupotezwa na yule mwovu nitawarudisha na wale waliodhoofu kiroho nitawatia nguvu"* (Ezekieli 34: 11 - 16)

Mungu anawaahidi kuwachukua kifuani mwake wale wadogo na wanyonyeshao atawaongoza pole pole. (Isaya 40: 11) Naye Kristo ndiye mchungaji mwema wa kundi hilo la Mungu na akawa tayari kuyatoa maisha (uhai) wake kwa ajili ya kondoo wake (Yoh 10:11 - 15, Pet. 5:4)

(b) Kanosa linafananishwa na Shamba la Mungu lenye kuzaa sana. Yeye analilima vizuri, anaotesha humo zabibu zilizochaguliwa na kuyajalia lizae. Shina lake latoka mbinguni na kuyajalia matawi yake (sisi wana Kanisa) unyenyekevu ili tuwe na uhai na uwezo wa kuzaa matunda mema, yaani utakatifu. (Isaya 5: 1-2)

(c) Kanisa ni jengo la Mungu, jengo hilo limo ndani mwetu. Paulo Mtume anawaambia Wakorintho *"Nyinyi ni jengo lake Mungu"* (1Kor. 3:9) Yesu ndiye jiwe la msingi (Zab. 118:22, Mt.4:11) kwa hiyo wokovu wetu haupatikani kwa mtu yeyote kwa maana duniani pote binadamu hawakupewa jina la mtu mwingine ambaye twaweza kuokolewa kwalo isipokuwa jina la Yesu Kristo. (Mdo. 4:12)

Jengo hilo limejengwa juu ya mwamba ambao hata kifo hakitalishinda. (Mt. 16:18) Limejengwa juu ya msingi wa mitume ambao Yesu aliwandaa miaka mitatu. Paulo anasema "Hakuna mtu awezaye kuweka msingi mwingine badala ya ule uliokwisha kuwekwa na Yesu Kristo. (1Kor. 3:1) jengo hilo liliwekwa chini ya Mtume Petro na Mahalifa wake na waandamizi wao na kulifanya liwe imara na lenye muungano thabiti.

(d) Kanisa linafananishwa na nyumba ya Mungu wanamoishi familia ya Mungu. (1Tim. 3:15). Nabii Ezekieli anafanisha Kanisa na Maskani ya Mungu katika Roho (Ez. 2:19 - 22) Maskani ya Mungu pamoja na wanadamu (Ufu 2:9) Mji Mtakatifu (Ufu.21:1) ni Yerusalemu ya juu (Ufu. 12:17)

Mtakatifu Thomas wa Akwimo anasema "Kanisa ni Mwili wa Kristo na ndani ya mwili huo uhai wa Kristo unapatikana kwa njia ya ubatizo ambao kwao waamini hufanywa mwili mmoja na Kristo (LG 6-7) (Ibara 291 - 303) Fumbo la Kanisa" Yote haya yanakamilishwa na Kanisa linakuwepo kwa uwepo wa waamini yaani Maaskofu, Mapadre, Mashemasi, Watawa wa kiume, wa kike, na Walei. Hawa ndio wanakanisa.

## 1.2 Kanisa la kweli

Kanisa la kweli lazima liwe na alama nne 1. Moja 2. Takatifu 3. Katoliki 4. La mitume

(i) Ni moja kwasababu mwanzilishi wake ni mmoja naye ndiye Kristo.

Yeye alimwambia Petro "Wewe ni mwamba na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu, wala mlango wa kuzimu hautalishinda. Nami nitakupa funguo za ufalme wa mbinguni lolote utakalofunga duniani litakuwa limefungwa mbinguni, na lolote utakalofunga duniani litakuwa limefungwa mbinguni, na lolote atalofungua duniani litafunguliwa mbinguni "

(ii) **Ni Takatifu**

Ni takatifu kwasababu mwanzilishi wake ni Mtakatifu Malaika Gabrieli alipomtokea mwanamwali Bikira Maria aliyekuwa mchumba wa Yosefu wa Ukoo wa Daudi alimwambia "*Mtoto atakayezaliwa ataitwa Mtakatifu Mwana wa Mungu*" (Luka 1:35).

(ii) **Ni Katoliki**

- (a) Ni Katoliki kwasababu Kristo yumo ndani yake Mtakatifu Ignasi anatuambia, "Palipo na Kristo ndipo lilipo Kanisa Katoliki. Ndani ya Kanisa hilo mna ujalifu wa mwili wa Kristo uliounganika. Mungu ameweka vitu vyote chini ya miguu ya Yesu Kristo. (Efe. 1:22-23).
- (b) Ni Katoliki kwa kuwa ni ya kuenea popote toka bahari hadi bahari na kwa mataifa yote. Nalo ni agizo la Yesu "*Nendeni ulimwenguni kote mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu, na kuwafunzisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi, tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote hata ukamilifu wa dahari*" (Mdo. 28:19-20.

(iv) **Ni la Mitume**

Ni la mitume kwasababu limejengwa juu ya mitume aliowaandaa Yesu kwa miaka mitatu na kuwatuma, "*Nendeni mkahubiri habari njema kwa kila mtu anayeamini na kubatizwa ataokolewa*". (Marko 16: 18 -16) Pia katakisimu ya Kanisa Katoliki (Ibara 118 - 870).

# SURA YA PILI

# MTAGUSO MKUU II WA VATIKANI:

Papa Yohane wa XXIII (Ishirini na tatu) alidokeza wazo la kuitisha mtaguso Mkuu II wa Vatikani na Mtaguso uliitishwa na kuzinduliwa rasmi tarehe 11.10.1962, baada ya sala na matayarisho ya kitaalam.

Papa Yohane wa XXIII alifariki tateh 03.06.1963 wakati Mtaguso Mkuu ukiendelea na Papa mpya Paulo wa VI, aliendeleza Mtaguso hadi ulipofungwa tarehe 08.12.1965.

Mtaguso ulikuwa na madhumuni ya kutoa dira mpya ya maisha ya Kanisa Katoliki, na hivyo kulifanya lianze Pentekoste mpya. Roho Mtakatifu aliwavuvia wazee wetu wa Kanisa mwanga na kanisa ya wanafamilia wote wa Mungu ulimwenguni. Mtaguso ukawa mhimili na mtetezi wa wanyonge. Mtaguso huo ulijadili hati 16, miongoni mwa hati hizo ilihusu Utume wa Walei na wajibu za Walei katika Utume wa Kanisa.

**2:0 MLEI**

**2.1 Mlei ni nini?**

(a) Neno Mlei limetokana na lugha ya Kigiriki "LAOS" maana yake raia, wananchi au taifa. Katika Kanisa linaelezea ni wakristo wa msingi, yaani waamini wasio na daraja takatifu la upadre au utawa. Mtaguso Mkuu wa II ndio uliotoa maelezo ya nafasi ya Mlei katika Kanisa. Ukitamka Walei sio tabaka fulani ndani ya Kanisa, bali Walei ni wana Kanisa sawa na Maklero (Maklero ni Maaskofu, Mapadre na Mashemasi) kwahiyo Walei ni viungo vya mwili wa Kristo ni taifa teule la Mungu mmoja, katika Bwana mmoja, katika imani moja na ubatizo mmoja. (Ef. 4:5) Mtaguso ulikazia kuwa wana Kanisa wote wana hadhi moja ya kuzaliwa upya-katika Kristo, wakiwa na Neema moja ya kuwa watoto wa Mungu, wenye wito mmoja wa kuifikia ukamilifu, wakipata wokovu mmoja, tumaini moja na upendo usiogawanyika (LG 32) Ibara ya 364 - 367 (Fumbo la Kanisa).

Maklero wanatekeleza utume wa Kanisa, wakiinjilisha kwa kuhubiri Injili kwa niaba ya Kanisa nzima (LG 19) ibara ya 330 (Fumbo la Kanisa Walei nao wanainjilisha kwa ushuhuda wa maisha yao ya imani na mapendao kwa Mungu na kwa jirani (LG 12) Ibara ya 316) (Fumbo la Kanisa).

(b) Mtume Mlei kwa ubatizo anakuwa mtume na Yesu mfuasi anayetumwa kwenda kwa mataifa kama mitume wengine wakatangaze Habari Njema, wakiwagawia watu Neema ya wokovu.

Mtaguso unawaagiza Walei washirikiane na viongozi wa Hierakea (Maaskofu, Mapadre, Mashemasi) na watawa (Mabradha na Masista) kutangaza Habari Njema. Unawasihi waifanye kazi hiyo kwa bidii na ujasiri mkubwa hata ikifikia kuutoa ushuhuda wao wa kufia dini kwa ajili ya imani yao kwa Mungu na Yesu Kristo. Walei watambue wao ni washiriki hai wa kiungo cha mwili wa Fumbo wa Kristo yaani Kanisa. Kwa kutimiza hayo wanahitajika kujirekebisha upya, wakirudisha uhusiano wao mwema na Mungu na kuishi maadili mema ya kumpendeza Mungu.

(c) Siku ile ya Pentekoste, Roho Mtakatifu aliwaondolea Mitume Walei na waamini wote woga na wasiwasi na kueneza Habari Njema. Hii ndiyo ile siku ya ahadi ya Yesu aliyoahidi kumpeleka Roho Mtakatifu ilipotimia. Mitume na wafuasi walipata nguvu ya kutangaza Injili. (Mdo. 2:4 - 36).

(d) Yesu Kristo aliweka Utume wa Walei mikononi mwao, wakitiishwa huo mzigo wenye heshima wa kueneza Injili ili azimio la wokovu la Mungu liwafikie watu wote wa nyakati zote na mahali pote duniani (LG 33) (ibara 371) Fumbo la Kanisa. Wafundishe imani Katoliki kwenye familia zao, jumuiya ndogondogo, shule za msingi, Parokia n.k. Wakifundisha upendo, Utii, Huruma, Msamaha na Uaminifu. Wakilea miito ya Upadre, Utawa na Ndoa safi, familia zao ziwe shule nao wakiwa waalimu.

## 2.2 UTUME WA WALEI

- Mtaguso Mkuu wa II wa Vatikani unatufafanulia Utume wa Walei kuwa ni kule kushiriki kwa Mlei, Utume wa Kanisa uletao wokovu.

  Ni kule kutimiza Utume huo ambao Walei wote wamepewa na Mungu mwenyewe kwa njia ya Ubatizo na Kipaimara. Kwa Ubatizo Mlei anakuwa mwana wa Mungu na Mfuasi wa Kristo, kwa Kipaimara Mlei anakuwa askari hodari wa Kristo aweze kumtangaza Mungu na Yesu Kristo yaani wanawekwa na kufanywa watendaji katika Taifa takatifu la Mungu wakimshuhudia Kristo mahali pote (AA3) Ibara 918 (Utume wa Walei)

**KAZI ZA KITUME AMBAZO MITUME WALEI HUZIFANYA**

Kazi za Kitume ambazo kwanza Walei wanajenga nazo Kanisa.

(i) Pale wanapojitoa kwa hali na mali na kwa kujitoa kwa kazi mbalimbali za kikanisa. Mtaguso anawaagiza Walei wazoea kufanya kazi bega kwa bega na Mapadre wao, wapende kujitoa kwa bidii na kwa uwezo wa kila mmoja kadri walivyo kirimiwa na Mungu wakifahamu Kigango au Parokia ni vya wana Kigango na Wanaparokia. Hivyo watunze Jimbo lao, Taifa lao na Kanisa la ulimwengu. Walei watambue kuna michango ya Kigango, Parokia, Jimbo, Taifa na ya Kimataifa (AA 10) Ibara 950 - 968 (Utume wa Walei).

(ii) Pale Walei wanapoonyesha uwepo wa Kristo katika hali zao za maisha wakimshuhudia Kristo kwa imani, wakamtangaza Mungu na Yesu Kristo wakifafanua, mafundisho yake na kuyaeneza kadri ya hali na uwezo wao na kuyakiri kiaminifu. Pale wanapositawisha mpango wa malimwengu kwenye maisha yao ya nyumbani, kazini, ya kiutamaduni na ya kijamii. (AA 16) Ibara 972 - 974 (Utume wa Walei). Malimwengu ni yale mambo ya kidunia wakiyafanya yaendane na mpango wa Mungu na amri zake.

(iii) Pale Walei wanapoishi wakivumilia kwa hiari magumu na mateso wanafananishwa na kuyabeba mateso ya Yesu Kristo Mteswa. Mtume Paulo anatuambia “Kila siku mwachukua miili yenu kwa kuuawa ili uzima wa Kristo udhiirishwe” (2Kor 4:10) Yeye mwenyewe anakiri “*Sasa nafurahia mateso niliyonayo nikitimiza katika mwili wangu yale yaliyopungua katika mateso ya Kristo na kwa ajili ya mwili wake yaani Kanisa” (Wakolosai 1:24).*Hivyo kwa matendo ya Walei kila siku, kwa sala zao kwa maisha yao ya ndoa na familia, kwa kazi ngumu za kila siku, kwa taabu za maisha, vyote wakivichukua kwa uvumilivu vinageuka dhabiu za kiroho zinazokubalika na Mungu kwa njia ya Yesu Kristo (1Pet. 2:5).

(iv) Pale Walei wanaposhiriki ibada za pamoja, Misa Takatifu, Kuabudu Ekarisiti. Njia ya msalaba, Rozali Takatifu, Sakramenti ya Upatanisho wanashiriki Utume wa Kanisa. Utume wa Walei katika Kanisa unafanikiwa kwa urahisi zaidi pale unapofanyika kama “UTUME WA PAMOJA” yaani ushirikiano. Yesu Kristo anasema, “Walipo wawili, watatu wamekusanyika kwa jina langu, nami nipo papo hapo katikati yao. (Mt. 18:20).

- **UHUSIANO WA WALEI NA VIONGOZI HIERAKIA NA WATAWA**

  Mtaguso unawahimiza viongozi Hierakia kutambua wajibu zao za kushiriki shughuli katika kujenga Kanisa Mwili wa Kristo, kindugu na viongozi wao kwa ajili ya Kanisa. Mapadre wasaidie Walei kuyafahamu mafundisho ya Kanisa ili wakuze maisha yao ya kiroho, wawe na mawasiliano ya kindugu na Walei wao, wawe na upamoja katika njia zile zinazoleta matunda mengi katika kazi za Walei za Kitume ili Walei wapate kustawisha roho ya umoja katika Kanisa na katika vyama vyao vya Kitume.

Watawa wa Kiume na wa kike wanaombwa na Mtaguso Mkuu wa Vatikani wasitahi matendo ya Walei wakiwaimarisha kulingana na katiba zao za Halmashauri Walei katika matendo hayo ya kitume, wawasaidie kwa moyo Walei katika matendo hayo yao, wakisimamia, wakiwasaidia waweze kukua kiimani wakishirikiana na viongozi Hierakia `(AA 25) Utume wa Walei. Mtaguso wawaambia Walei kuwa nao wanapaswa kuwa na uhusiano mwema na viongozi wao wa Hierakia na wakipokea kutoka kwao Neno la Mungu na Sakramenti mbalimbali. Walei wanashauriwa wawajulishe wachungaji wao mahitaji yao na matakwa yao kwa uhuru na matumaini wakiwa kama mwili ulivyo na viungo vingi kila kimoja kikihusiana na kiungo kingine ili kuujenga mwili mmoja, kukiwa hakuna utengano (1Kor 12: 20, 25 - 27).

## 3.0 WALEI NA UONGOZI NDANI YA KANISA

3.1 Baraza la Maaskofu Katoliki (TEC) walitafsiri hati zote 16 za Mtaguso Mkuu wa II wa Vatikani na kuanza kuzifanyia kazi. Hati ya Utume wa Walei ilianza utekelezaji wake mwaka 1968 kwa kuandaa KATIBA YA BARAZA LA WALEI TANZANIA, na uchaguzi wa viongozi Walei zilianza mwaka 1969. Viongozi waliochaguliwa kuanzia Parokia, Jimbo na Taifa.

Mwaka 1979 Maaskofu Katoliki Mashariki mwa Afrika (*AMECEA)*(Association of Member, Episcopal Conference of Eastern Africa) walitamka kuwa "Hakuna njia nzuri na mahususi ya kufanya Kanisa KATOLIKI Mashariki mwa Afrika limwilishe tamaduni nzuri za watu na kuliwezesha kujitegemeza KUIENEZA INJILI, KIUTUMISHI NA KIUCHUMI isipokuwa kwa njia ya JUMUIYA NDOGONDOGO ZA KIKRISTO.

i. Katika Jumuiya Walei wafundishe Injili "Kuhubiri Injili kwa kila kiumbe, aaminiye ataokoka" (Marko 16: 15-16)

ii Katika Jumuiya Walei waongoze wenzao: *Kama vile Mwana wa Adamu (Yesu) hakuja kutumikiwa bali kutumikia na kutoa nafsi yake iwe jidia ya wengi (*Mt. 2:28)

(iii) Kiuchumi yaani Walei wachangie kwa hali na mali kadri Mungu alivyowakirimia ili kulitegemeza Kanisa "leteni malimbuko Sadaka zenu na matunda ya miti, mvinyo na mafuta kwa makuhani, nyumbani mwa nyumba ya Mungu wenu, Zaka za ardhi na mifugo ya wanyama. Semeni sisi hatutaiacha nyumba ya Mungu, Mungu wetu ikae katika hali ya kuharibia " (Nehemia 10: 37 -39)

Nabii Hagai anasema, "Mlitazamia vingi kumbe mkavuna vichache, tena mlipovileta nyumbani nikavipeperusha. Ni kwa sababu gani, asema Bwana wa Majeshi. Ni kwasababu ya nyumba yangu inayokaa katika hali ya kuharibika, wakati nyinyi mnakimbilia kila mtu nyumbani kwake" (Hagai 1:9). Atazuia Mbingu zisitoe umande, nchi isitoe matunda kama hatutoi ipasavyo ili kulitegemeza Kanisa.

Katika kutekeleza tamko la Maaskofu hao wa AMECEA, Maaskofu Katoliki Tanzania walianza kuunda Jumuiya ndogondogo za Kiristu na Baraza la Walei likawa linaanza chaguzi za viongozi kuanzia JNNK hadi Taifa. Katiba ya Baraza la Walei Tanzania iliendelea kuongoza hadi mwaka 2000 tulipoadhimisha Jubilei Kuu miaka 2000 tangu kuzaliwa kwa Bwana wetu Yesu Kristu. Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania walipoona umuhimu wa kuwa na marekebisho ya katiba ya Baraza la Walei iliyoanza mwaka 1969.

Mwaka 2004 tarehe 6 Januari Katiba mpya ilitangazwa rasmi yenye jina Halmashauri ya Walei Tanzania.

(i) Ni chombo cha kuwaunganisha Walei wote kutoka Jumuiya ndogondogo za Kikristo, vijiji/Mtaa kanda, Vigango, Parokia, Jimbo na Taifa.
(ii) Ni chombo cha kitume kinachoundwa kwa ajili ya kushauri juu ya ustawi wa UTUME wa Walei na kinaendeshwa na Walei wenyewe wanaochaguliwa kihalali kulingana na Katiba na ushauri wa jumla wa

viongozi Hierakea agizo la Mtaguso Mkuu (AA 20) Ibara (1992 -1993) Utume wa Walei.

## 3. UONGOZI WA WALEI NDANI YA KANISA

### (a) UONGOZI NI NINI?

Uongozi ni ile nafasi anayopewa mtu kwa kutumiwa "UWEZO" wake akawaongoza, waongozwa kufikia malengo yaliyotarajiwa. Uwezo upo katika maneo au matendo au vyote kwa pamoja, uongozi nao una sehemu mbili:

1. **Uongozi mzuri:** (Huyu tunamwita kiongozi bora) Kikanisa huyu atawaongoza watu kuupata wokovu wanaouwania (Ufalme wa Mbinguni).

2. **Uongozi mbaya:** (Huyu tunamwita kiongozi mbaya kwani hatawafikisha waongozwa kufikia malengo yaliyotarajiwa) Kikanisa atapeleka watu motoni, Yesu anasema, "Kipofu akimwongoza kipofu mwenzie wote wawili watumbukia shimoni" (Mt 15:14)

**MUNGU HUTENGENEZA VIONGOZI WAKE:**

Tunajifunza haya kwa Musa, Mungu alimwita Musa na kumwambia, "*Nakutuma kwa Farao Mfalme wa Misri, ukawatoe watu wangu nchini Misri, watu hao ni Waisraeli"*

Musa hakuamini kuwa ana uwezo wa kuongea na Farao Mfalme wa Misri, wala uwezo wa kuwaambia hao Waisraeli lengo lake la kuwatoa nchini Misri na anawapeleka wapi, ndipo anamjibu Mungu "*Mimi ni nani hata niende mbele ya Farao Mfalme wa Misri niwatoe Waisraeli nchini Misri? Je, hao Waisraeli watanielewa? "(*Kut. 3: 10 - 11).

Mungu aliona jambo fulani kwa Musa, nalo ndilo analotamani kulitumia.

Hivyo Mungu anamwambia Musa "*Bila shaka mimi nitakuwa pamoja nawe katika kumwendea Farao na katika kuongea na hao Waisraeli" (*Kut. 3:12) Mungu alimtengeneza Musa awe chombo chake cha Ukombozi.

Tunajifunza kwa Yeremia "Mungu anamwambia Yeremia, "Kabla sijakuumba katika tumbo nalikujua na kabla hujatoka tumboni nalikutakasa uwe Nabii wa mataifa" Yeremia anajibu, "*Aaa Bwana Mungu! Tazama siwezi kusema maana mimi ni mtoto,* "Bwana akamwambia, "*Usiseme mimi ni mtoto maana utakwenda kila mahali nitakapokutuma nawe utasema kila neno nitakalokuamuru.* "Usiogope kwa sababu ya hao maana mimi nipo pamoja nawe. Ndipo Bwana akanyoosha mkono wake akamgusa Yeremia kinywa chake na kumwambia "**TAZAMA NIMETIA MANENO YANGU KINYWANI MWAKO" (Yer. 1: 5-9).**
Mungu huwatengeneza viongozi wa kufanya yale atakayo yafanyike na kufanikisha pamoja na wote wampendao yaani wale aliowaita kadri ya kusudi lake. (War. 8:28)

**(B) UONGOZI KATIKA KANISA**

Uongozi katika Kanisa ni Utumishi, ni huduma sio mahali pa kujipatiza marupurupu. Anatazamiwa awe kiongozi bora. Kiongozi bora ni yule anayetambua wajibu wake, anayejituma, na anyemshirikisha Mungu yale anayoyafanya. Ni yule anayewaongoza wenzake kuzijua njia za kuwaelekeza na yeye mwenyewe akiwa mstari wa mbele na wenzake wakimfuata.

Baadhi ya watu wamezaliwa na vipaji na sifa za uongozi bora wengine wakitengenezwa na Mungu, wengine wakiwa viongozi bora kwa:-

(i) Kutaka ndani mwake, yaani kuwa na nia ya kuongoza
(ii) Kujifunza kutoka kwa Viongozi bora
(iii) Kuomba ushauri kutoka kwa viongozi Hierakea.
(iv) Kushiriki Semina na mikutano mbalimbali
(v) Kujisomea vitabu, magazeti na vipeperushi vinavyoeleza juu ya uongozi.

Vingozi wa Kanisa wanapaswa wawe chumvi na mwanga kwa wale wanaowaongoza (Mt. 5:13 -16) Wawe kielelezo kizuri kwa wengine (Luka 6:39). Aonekane kama kioo kwa wale wanaomtazama. Uongozi katika Kanisa lazima uongozwe na kuimarishwa na Roho ya Injili.

Awe na Sifa zifuatazo:-

**(C) SIFA ZA KIROHO**

1. Awe msomaji wa Neno la Mungu (Biblia) na kutafakari. Neno la Mungu humfanya Kiongozi kukua Kiroho, tena ni taa ya miguu yake na mwanga wa njia yake (Zab. 119: 105). Kutokusoma neno la Mungu kunamfanya kiongozi kudumaa kiroho, kuwa na "UKIRO" (upungufu wa kinga rohoni). Kiongozi wa namna hiyo huwaongoza waongozwa motoni badala ya mbinguni.
2. Awe anashiriki Liturujia ya Ekarisiti (MISA) Jumapili na siku za amri.
3. Awe anashiriki Ekarisiti Takatifu mara kwa mara na kushiriki Sakramenti ya Upatanisho.
4. Awe anaishi kiaminifu ndani ya ndoa na nje ya ndoa kwa wenye ndoa na wasio na ndoa.
5. Nyumba yake iwe kikanisa kidogo cha sala (KKK 2685) shule

ya Imani, huruma, utii, mapendo na matumaini. Mahali pa kulea miito ya Upadre, Utawa na ndoa safi.

## (D) SIFA ZA KIUTENDAJI

Hizi ni sifa za mwili, za akili, kitaalamu na kitabia

1. **Kumwamini Mungu** Kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo kati ya mambo yasiyoonekana (Ebr. 11:1). Abraham anaambiwa "Toka hapa wewe katika nchi yako uende mpaka nchi nitakayo kuonyesha iwe Urithi wako nami nitakufanya taifa kubwa na kulikuza jina lako" (Mwa. 12:1-4) Abrahamu kwa kuamini hakuna lisilowezekana kwa Mungu aliondoka.

   Abrahamu akampokea kwa furaha mtoto Isaka katika uzee wake, Mungu akamwambia "Mchukue mwanao umpendaye Isaka ukamtoe sadaka ya kuteketezwa. Kwa imani akamchukua na kumweka tayari kwa sadaka. Mungu aliona imani yake akambariki" (Mwa. 22:1-18)

   Bikira Maria anaambiwa "Tazama utachukua mimba na kuzaa mtoto mwanaume utamwita jina lake Yesu". Maria akauliza "Litakuwaje neno hili maana mimi simjui mume" Maria anajibiwa "Roho Mtakatifu atakushukia na kitakachozaliwa kitaitwa kitakatifu Mwana wa Mungu. Maria kwa Imani kwa Mungu akasema "Mimi ni mtumishi wa Bwana na iwe kwangu kama ulivyosema "(Luka: 1:31-38)
2. **Kujiamini na Kuamini wengine:** Kiongozi lazima ajiamini kuwa anaweza kuongoza waamini wale anaowaongoza.
3. **Uhusiano mwema:** Kiongozi lazima awe na mahusiano mema na viongozi wenzake na viongozi wa Hierakea.
4. **Kutumika:** Kiongozi lazima awe tayari kutumikia wale anaowaongoza. Yesu anasema "Mavuno ni mengi, wavunaji wachache, mwombeni Bwana wa mavuno apeleke watenda kazi katika mavuno yake (Luk. 10:2) Kielelezo ni Yesu, yeye hakuja atumikiwe bali atumika (Mt. 20:28)

5. **Kujitolea:** kiongozi lazima awe mtu wa kujitolea, awahimize anaowaongoza kujitolea. Mtaguso unawahimiza Walei wajitolee katika kufanya kazi bega kwa bega na Mapadre wao. (AA 10) (Ibara 950 Utume wa Walei).

6. **Kuwa na Upendo, Uvumilivu na Unyenyekevu:** Kuwapenda wote bila ubaguzi wa rangi, jinsia, cheo n.k. Kuwa na uvumilivu kwa yanayoweza kutokea, kashfa, masengenyo, kuwaziwa vibaya n.k. Kunyenyekea wote na kutii viongozi Hierakea na waongozwa.

7. **Kuwa msiri:** Kiongozi lazima ayasitiri madhaifu ya watu, asiwe mpepetaji, akawavunja wengine moyo katika imani.

8. **Kuwa Mshirikishaji:** Kiongozi lazima awashirikishe wale anaowaongoza yale anayoyafanya na kushirikisha viongozi Hierakea.

9. **Kuwa na mtazamo mpana:** Kiongozi lazima awe mbunifu wa mambo yatakayoleta maendeleo ya Halmashauri Walei Chama cha Kitume ngazi zote *JNNK, KIGANGO, PAROKIA, JIMBO, TAIFA NA JAMII INAYOWAZUNGUKA.*

10. **Kuandaa Viongozi:** Ni vema na ni haki kuwandaa Viongozi watakaoendeleza Halmashauri Walei au Chama cha Kitume ngazi zote baada ya wewe kuacha uongozi kwa sababu yoyote ile mfano: uhamisho, Uzee, Ugonjwa na Kifo n.k.

## (E) WAJIBU WA JUMLA WA VIONGOZI:

1. Kudumisha utume wa Walei kwa kuimarisha maisha ya kiutakatifu miongoni mwa Walei.
   (a) Kwa kuwahimiza Walei kujenga Mwili wa Kristo yaani waishi pamoja kindugu (Mdo. 2: 2 - 46).

(b) Kuwahimiza Walei kuutafuta na kuufikia utakatifu yaani waupate uzima/Ufalme wa Mbinguni.

2. (a) Kustawisha Utume wa familia na Uinjilishaji wa Kina.
(b) Kuhakikisha familia unazoziongoza zimeimarika kiutendaji na kimaadili.
(c) Familia unazoziongoza zitambue kuwa katika familia ndimo utakatifu unamojengwa. Kila anayezaliwa humo atambulike ni zawadi ya familia (Zab. 127:3). Ni mahali pa kulea imani, ni shule ya sala/dini (KKK 2685) shule ya Upendo, Utu, Utoaji na maadili mema.
(d) Kuzifanya familia zikwepe matendo yasiyoendana na mapenzi ya Mungu.
   (i) Kusiwepo na washirikina
   (ii) Kusiwepo walevi wa kupindukia, wanywa gongo, wavuta bangi na wenye kutumia madawa ya kulevya

3. Kushauri Walei kushiriki Ujenzi wa Kanisa mahalia. Ushauri unaowaongoza njia mbalimbali za kujipatia kipato halali kwa ajili ya matumizi yao binafsi, kuchangia maendeleo ya Kanisa kwa manufaa ya wanakanisa na jamii inayo kuzunguka, mfano kujenga chekechea, chuo cha ufundi, zahanati, mashine ya kusaga n.k. Wewe kiongozi ukiwa mstari wa mele katika kuchangia.

4. Kudumisha Moyo wa Sala na Ibada miongoni mwa Walei unaowaongoza wajue kusali ni kuongea na Mungu, ni kuinua mioyo na roho zao kwa Mungu (KKK 2590) Wawe na sala za maombi kwani tunayo mengi tunayohitaji kutoka kwa Mungu, kwa Yesu kwa Roho Mtakatifu, kwa malaika walinzi, kwa watakatifu n.k. Tunajifunza kutoka kwa Yesu, hakufanya lolote bila kusali kwanza:
(a) Kabla ya kuteua Mitume alienda mlimani ili kuomba akakesha usiku kucha. (Luka 6:12-16)

(b) Alipokaribia kukamilisha kazi yake alienda katika bustani ya mizeituni kuomba (Mt. 26:36 - 39)
(c) Anatuombea katika yote (Yoh. 17: 1-26)
(d) Anatuhimiza "Ombeni nanyi mtapewa, tafuteni nanyi mtaona, bisheni nanyi mtafunguliwa. (mt. 7:7-11)
    (i) Wawe na Sala za kushukuru (Zab. 105: 1 -5)
    (ii) Kuwe na Sala za kumsifu Mungu. Tunashauriwa "Umsifu Mwenyezi Mungu ee nafsi yangu" (Zab. 104:1)

5. Kustawisha vikundi mbalimbali vya kitume katika eneo lako. Kuhakikisha kuwa kuna wanachama wa Vyama Mashirika /Jumuiya ya Kitume kuanzia JNNK hadi Parokia, Jimbo na Taifa. Kanisa linashauri watoto wote walioanza chekechea lazima wajiunge na Shirika la Utoto Mtakatifu wa Yesu, huko watapata malezi bora na kujifunza sala na nyimbo za kidini.
    - Wakishapata Komunyo ya kwanza, wa kiume wajiunge na Shirika la Mt. Aloisi na wa kike Bikira Maria. Huko wataendelea kupata malezi na kuilea miito yao.
    - Wakifikia ujana wajiunge na Vyama vya vijana mashuleni TYCS na VIWAJIMO (Vijana wa Wakatoliki Wafanyakazi
    - Wakifikia Kuoa/Olewa wa kiume wajiunge na Shirika la Mt. yosefu, huko atapata mafundisho jinsi ya kulea familia Takatifu, aombe maombezi ya Mtakatifu huyo.

Wa kike ajiunge na shirika la Mt. Anna, atajifunza kutoka kwa Mt. Anna, Mt. Monika, Bikira Maria namna njema ya malezi na kuombea watoto wao.

- Uzeeni wajiunge na Shirika la Mt. Augustino (Wazee na Wastaafu) wapate nafasi ya kumshukuru Mungu kwa uhai, maisha, mapaji aliyowakirimia na kuomba kifo chema.

  Kuna Vyama na Mashirika mengine kama moyo Mt. wa Yesu, Legio Maria, Kazi za Roho Mtakatifu, Wafransisco, Wasekulari n.k . Ni wajibu wa kila kiongozi kushauri watu anaowaongoza wajiunge, naye awe mmojawapo wa wanachama ili ajitafutie utakatifu na kutaka kufuza wengine.

6. **Kuhamasisha Shughuli za Maendeleo**

(i) Kuhimiza watu wafanye kazi kwa bidii na kwa kitaalamu wajipatie kipato badala ya kuwa wazururaji, wakaaji kijiweni, wakinywa gongo, wakitumia madawa ya kulevya n.k.

(ii) Kuwahimiza Walei washiriki mambo ya siasa wakipenyeza "Ukristo" wao ndani wakikemea rushwa na dhuluma ipatikanayo kwa njia zisizo halali (Isaya 33:15) wakiwa sauti kwa wasio na sauti, wakitetea wazee, wajane, mayatima, walemavu, watoto n.k wapate haki msingi zinazowapasa.

(iii) Kuhamasisha walei unaowaongoza waanzishe/ wajiunge na vikundi vitakavyowaletea maendeleo kama SACCOS au VICOBA (Village Community Bank) waweze kuweka hisa zao na kukopa kwa wakati hitaji.

7. **Kuhimiza Utumiaji wa miundo inayokubalika na Kanisa katika kulinda na kutetea uhai.**

(i) Watu wajue kutoa mimba ni kuua, tena ni dhambi ya mauti, watambue damu ya viumbe hivyo inamlilia Mungu, na siku ya mwisho wataulizwa, "Umefanya nini? (*Mwa. 4:10)*

(ii) Wajue haki za binadamu kama vile haki ya kuishi, kuheshimiwa, kudhaminiwa, kusamehewa, kuhurumiwa, n.k.

8. **Kushirikiana na Viongozi Hierakia ngazi zoe katika kutekeleza majukumu ya Kanisa.**
Walei washirikiane bega kwa bega na viongozi wao wa kiroho katika majukumu ya Kanisa bila kusema hili ni la Padre hili ni la Mwenyekiti wa Parokia/Kigango bali washirikiane na kuwajibika. Katika Kanisa kila Mlei anapaswa atende kadri ya uwezo aliokirimiwa na Mwenyezi Mungu. Watambue agizo la Mtaguso. (AA 10:950 - 95)

**WAJIBU WA KIONGOZI MMOJA MMOJA:**

- **MWENYEKITI**

(i) Kuongoza mijadala katika mikutano akizingatia:-
- (a) Kuwahi kabla ya wote ili akishirikiana na Katibu waone yote yapasayo kuwemo kwenye mkutano yamekamilika, akizingatia muda ulipangwa katika ratiba.
- (b) Kutoa nafasi sawa kwa kila mzungumzaji au mtoa hoja bila upendeleo.
- (c) Kuheshimu na kupokea maoni ya wengi yaani "Demokrasia"
- (d) Kutumia lugha safi, maneno yanayoeleweka, maelezo yaliyo sahihi na mifano inayofaa.

(ii) Kutayarisha Dondoo (Agenda) kwa ushirikiano na viongozi, Kamati tendaji na hasa katibu.

(iii) Kutoa neno au uamuzi wa mwisho baada ya majadiliano katika masuala fulani kadri ya busara yake au kwa kuomba ushauri kwa viongozi Hierakia katika Kigango/Paroko/ Wakili Paroko.

Katika Vikarieti - Vikari / Katibu wa Vikari katika Jimbo Mkurugenzi wa Idara ya Utume wa Walei / Askofu.

Katika Taifa - Katibu Mtendaji TEC / Askofu wa Idara ya Utume wa Walei (TEC)

(iv) Kufuatilia utekelezaji wa maazimio /mapendekezo yakiwemo yatokanayo na kikao/mkutano.

(v) Kupokea maelezo (miongozo) kutoka kwa viongozi wa Kanisa - Padre, Askofu, Papa kwa utekelezaji

(vi) Kutoa taarifa ya kikundi anachoongoza kuhusu yaliyotekelezwa na yanayotarajiwa

(vii) Kushirikiana na viongozi wa Vyama, Mashirika na Jumuiya za Kitume kwa kuhakikisha vipo, akivishauri, akivitia moyo
na kuviimarisha pale inapobidi.

- **MAKAMU MWENYEKITI:**
  **Majukumu**
  (i) Anafanya yote anayofanya Mwenyekiti akimsaidia shughuli zote za uongozi ngazi husika.
  (ii) Anachukua nafasi ya Uenyekiti akifanya shughuli zote zinazo mhusu Mwenyekiti wakati hayupo isipokuwa kama kuna zinazokatazwa na Katiba.

- **KATIBU:**
  Huyu ni Mtendaji mkuu wa shughuli zote za Halmashauri Walei, Vyama, Mashirika na Jumuiya za Kitume.

**Majukumu:-**

(i) Kuijua na kuieleza kwa ufasaha katiba ya Halmashauri Walei Chama /Shirika/Jumuiya ya Kitume bila kupoteza lengo

(ii) Kumshauri Mwenyekiti ili mawazo yao yalingane.

(iii) Kutayarisha dondoo (agenda) za vikao na mikutano akishirikiana na viongozi kamati tendaji na hasa Mwenyekiti.

(iv) Kuitisha mikutano /vikao kwa kuandika barua akizingatia agizo la katiba. Kutoa taarifa kwa viongozi mbalimbali wanaohusika kupewa taarifa au kualikwa kuhudhuria.

(v) Kama kuna Semina, anaandaa kwa ushirikiano na Kamati Tendaji, Wakufunzi, Mgeni rasmi wa kufungua na kufunga.

(vi) Kuandaa chumba cha mkutano au Semina akihakikisha kuna viti vya kutosha, vifaa vya kuandikia, ubao, karatasi, makabrasha, kalamu n.k.

(vii) Kuwakaribisha wageni na kuwaelekeza mahali pa kukaa.

(viii) Kuandaa muhtasari wa vikao na mikutano na kuwasomea wajumbe katika vikao na mikutano iliyopita ili kuwakumbushia yaliyojadiliwa na yaliyotekelezwa na namna ya kutekeleza yale ambayo bado kwa ufanisi zaidi.

(ix) Kushughulikia barua zote za kiofisi

   (a) Kuhakikisha yaliyoagizwa kwenye barua yamewafikia walengwa

   (b) Zinazohitajika kujibiwa zimejibiwa ipasavyo.

   (c) Kuzihifadhi katika majalada

(x) Kuhifadhi na kutunza kumbukumbu za Halmashauri ya Walei, Vyama, Mashirika, Jumuiya za Kitume. Idara ya Utume ya Walei, Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC) wanahimiza kumbukumbu zote zihifadhiwe kwa mtu binafsi, kumekuwepo matatizo ambayo ni upotevu wa kumbukumbu kwa kung'ofolewa kwa makusudi na kupoteza malengo / uhakika.

(xi) Kufuatilia Utekelezaji wa maazimio / mapendekezo yote yaliyopitishwa katika vikao/mikutano na ya Kanisa.

- **KATIBU MSAIDIZI**

**Majukumu**

(i) Kumsaidia bega kwa bega Katibu katika kazi zote za ukatibu.
(ii) Kuchukua nafasi ya Ukatibu wakati Katibu hayupo.
(iii) Kupokea maelezo kutoka kwa Katibu na kuyatekeleza.

- **MTUNZA HAZINA:** Sifa kuu ya Mtunza Hazina ni kuwa *"MWAMINIFU, KUSOMA, KUANDIKA NA KUHESABU"*

**Majukumu**

(i) Kutunza mali, fedha za kikundi na kuweka kumbukumbu zake.
(ii) Kuweka hesabu za mapato na matumizi zikionyesha salio anzia, fedha zinazopatikana, matumizi yaliyokuwepo na salio bakia.
(iii) Kubuni mipango na mbinu za kuzalisha mali kwa ushirikiano na kati tendaji na ushauri wa viongozi Hierakea.
(iv) Kufuatilia utekelezaji wa maazimio ya vikao na mikutano yanayohusu fedha na miradi.
(v) Kutoa taarifa ya fedha yaani mapato, matumizi na vitu vya vikundi katika vikao/mikutano.

Idara ya Utume wa Walei Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania inashauri na kusisitiza taarifa ya fedha itolewe kila baada ya miezi mitatu (3) April, Julai, Septemba na Desemba

**UTARATIBU WA MIKUTANO KWA UJUMLA:**

Yafuatayo ni mambo ya kuzingatia wakati wa kuongoza/kushiriki mkutano.

1. Kugawa karatasi za agenda na ratiba (*katibu)*
2. Kupeana taarifa mbalimbali kama zipo, salamu, pongezi, matashi mema kutoka kwa labda Mgeni rasmi mwalikwa, vikari, Askofu n.k.

3. Kufunga mkutano kwa sala, Neno kutoka maandiko Matakatifu, Tafakari fupi na Neno la Ufunguzi.
4. Wajumbe kurithiwa dondoo (Agenda).
5. Kujitambulisha iwapo kuna washirii au mgeni mwalikwa na ni mara yake ya kwanza kushiriki.
6. Kusoma muhtasari wa kikao/mkutano uliopita, kufanya masahihisho na baada ya kukubaliana na wajumbe, Mwenyekiti na katibu hutia sahihi zao.
7. Kuzungumza yatokanayo na mkutano huo uliopita, yaliyohitaji utekelezaji kuona yalivyofikiwa.
8. Kujadili dondoo (agenda ) za siku hiyo moja baada ya nyingine. Kila mjumbe anapaswa:-
   (a) Kuwa msikivu kwa kila kinachozungumziwa ili aweze kuelewa na kutoa mchango wake wa mawazo, maoni au hoja.
   (b) Kuzungumzia maoni au hoja kwa kifupi bila kurudiarudia ili kuokoa muda.
   (c) Kuuliza maswali yanaohusiana na hoja au agenda
   (d) Kumrudisha msemaji anayekuja nje ya agenda.
   (e) Daima zungumza kwa ruhusa ya Mwenyekiti.
9. Kuweka "**MAAZIMIO**" Inashauriwa kuwa na kamati ndogo ya kuratibu mapendekezo ya maazimio ya mikutano.
10. Kupanga au kukumbushia tarehe ya mkutano ufuatao.
11. Ni ilani na ushauri kwa Mwenyekiti
   (i) Asizungumze mno wakati wa majadiliano bali atoe nafasi zaidi kwa wajumbe, tena bila upendeleo ili aweze kutoa uamuzi wenye busara.
   (ii) Asiruhusu mno wajumbe kurudiarudia hoja au kuunga mkono.
   (iii) Awavumilie na kuwaelekeza wasemaji wasiofuata taratibu za kawaida za mikutano au wenye lugha isiyopendeza

(iv) Aahairishe kikao anapoona wajumbe wanavutana katika hoja fulani bila kufikia maafikiano au uamuzi ili wajumbe wapate nafasi ya kutafiti na kutafakari zaidi nje ya chumba cha mkutano.

(v) Asizime maswali ya wajumbe, bali ayapokee na kikao kiyafanyie kazi.

(vi) Asiwe wa kwanza kuyajibu maswali ya jumla, bali awasihi wajumbe wachangie kujibu au kutoa maelezo zaidi na yeye awe wa mwisho kuchangia.

(vii) Azingatie muda uliopangwa kuepuka kuwachosha wajumbe

(viii) Demokrasia itumike katika kupiga kura, kila mjumbe akiwa na haki ya kura moja. Mwenyekiti ana haki ya kuwa na kura ya turufu ikiwa wapiga kura wamelingana kwenye kura.

Iwapo kila mjumbe atazingatia yaliyoainishwa hapa washiriki watafurahia vikao na mikutano kwani vikichukua muda mrefu bila sababu vinachosha na kukatisha tamaa ya kuhudhuria.

**KAMATI NDOGONDOGO ZA HALMASHAURI WALEI:**

Halmashauri Walei katika Kigango/Parokia, Jimbo/Taifa itakuwa na kamati ndogondogo nazo ni:

1. Mipango, uchumi na fedha
2. Malezi ya familia
3. Elimu ya dini, Mafundisho ya Kanisa na Teolojia
4. Haki na Amani
5. Liturujia.

A. **MPANGO , UCHUMI NA FEDHA:**
Mwenyekiti wa kamati hii ni MTUNZA HAZINA wa Kamati tendaji ngazi yoyote ile.
Atakuwa na wajumbe wanne (4) watakaoteuliwa na wajumbe kutoka Halmashauri ya Utekelezaji ambayo ni Wenyeviti wote kutoka Jumuiya ndogondogo za Kikristu, mtaa/vijiji, kanda, vigango, Parokia, Jimbo na Taifa na wenyeviti wa vyama/ Mashirika ya Kitume eneo husika. Paroko/Katibu Mtendaji /Mkurugenzi ni Mjumbe.

**Majukumu ya Kamati:**

1. Kusimamia mali na fedha za Halmashauri Walei na Kanisa wakizingatia ushauri wa Paroko, Mkurugenzi Utume wa Walei Jimbo na Katibu Mtendaji Idara ya utume wa Walei Baraza la Maaskofu Katoliki (TEC).
2. Kubuni mikakati ya kupata fedha kuendesha Halmashauri Walei na Kanisa Mahali.
3. Kutengeneza bajeti ya Halmashauri Walei na Kanisa wakiweka mpango mkakati kuanzia Jumuiya ndogo ndogo/Kigango na Taifa.
4. Kudhibiti matumizi Halmashauri Walei na Kanisa.

B. **MALEZI YA FAMILIA:**
Mwenyekiti wa kamati hii ni MWENYEKITI wa kamati tendaji ngazi yoyote ile. Wajumbe wanne (4) watateuliwa kutoka Halmashauri ya Utekelezaji ambayo ni wenyeviti wote kama namba moja. (Mipango, uchumi na fedha) Paroko/ Katibu Mtendaji /Mkurugenzi wa Idara ya uchungaji au Padre mlezi eneo husika anaalikwa.

**Majukumu ya Kamati:**

1. Kuratibu na kusimamia malezi ya familia, vijana na watoto kwa njia mbalimbali
2. Kuhamasisha uanzishaji na uendeshaji wa shule za awali.

3. Kuratibu mafundisho na malezi ya watu wa ndoa, kabla na baada ya kufunga ndoa.

4. Kuratibu na kusimamia mafundisho ya uzazi wa mpango kulingana na mafundisho ya Kanisa Katoliki

5. Kushauri kwa Ushirikiano na Paroko katika masuala ya ndoa na familia.

**C. ELIMU YA DINI, MAFUNDISHO YA KANISA NA TEOLOJIA**

Mwenyekiti wa kamati hii ni KATIBU MSAIDIZI wa kamati tendaji. Wajumbe wanne (4) watateuliwa kutoka Halmashauri ya Utekelezaji ambayo ni Wenyeviti wote kama namba moja (Mipango Uchumi na Fedha), Paroko, Katibu Mtendaji, Mkurugenzi wa Idara ya Elimu au Padre Mlezi eneo husika anaalikwa.

**Majukumu ya Kamati:**

1. Kuwezesha ufudishaji wa Biblia Takatifu na maandiko mengine yanayohusu Kanisa.
2. Kufuatilia ufundishaji wa Sakramenti mbalimbali za Kanisa.
3. Kuwezesha na kusimamia EKUMENI (Mahusiano ya Kanisa Katoliki na Madhehebu ya Kikristo na Dini nyingine).
4. Kuratibu mafundisho ya dini mashuleni.

**D: HAKI NA AMANI:**

Mwenyekiti wa Kamati hii ni KATIBU wa Kamati tendaji ngazi yoyote ile. Wajumbe wanne (4) watateuliwa kutoka Halmashauri Walei ambayo ni Wenyeviti wote kama namba moja (Mipango, Uchumi na Fedha) Paroko/Katibu wa Kamisheni na Haki na Amani ngazi husika anaalikwa.

**MAJUKUMU YA KAMATI**

1. Kuratibu ufundishaji wa Mafundisho ya Kanisa kuhusu jamii.
2. Kubuni Programu za kuwawezesha roho ya Injili kupenyeza katika malimwengu (malimwengu ni mambo yote ya maisha yanayohusu familia, kiuchumi, kiutamaduni, kisiasa na mahusiano ya taifa na mataifa).
3. Kuratibu na kufundisha Haki na Wajibu mbalimbali za watu.

**E. LITURUJIA NA IBADA:**

Mwenyekiti wa Kamati hii ni MAKAMU MWENYEKITI wa kamati tendaji ngazi yoyote ile. Wajumbe wanne (4) watateuliwa kutoka Halmashauri ya utekelezaji ambayo ni Wenyeviti wote kama namba moja (Mipango uchumi na fedha) Paroko, Katibu mtendaji, Mkurugenzi wa Idara Uchungaji au Padre mlezi anaalikwa.

**Majukumu**

1. Kuratibu Ufundishaji wa sala na ibada mbalimbali za Kanisa Katoliki.
2. Kupanga na kusimamia shuhguli za huduma Kanisani.
3. Kuongoza Sala na tafakari ya Neno la Mungu.

NB: Mjumbe yeyote wa Kamati ndogo ndogo haruhusiwi kuhudumia zaidi ya kamati moja isipokuwa anaweza kuhudhuria kikao kama mwalikwa kuhusu jambo fulani muhimu.

**MAJARIBU KATIKA UONGOZI:**

Majaribu ni matokeo ya mpatayo mtu katika dunia hii iliyojaa madhambi, madhulumu na inayoonekana kama imevunjika vipande vipande.

**(a) Majaribu mengine ni kwa mpango wa Mungu:**

- Abraham umtoe mwanao wa pekee Isaka umpendaye sadaka ya kuteketezwa. Abrahamu akamfunga Isaka na kumweka juu ya kuni tayari kumtoa lakini Mungu akamwambia, "Usimdhuru mtoto wala usifanye jambo lolote. Sasa najua kwamba unamcha Mungu kwani hukuninyima hata mwanao wa pekee (Mwa. 22: 1-12)

- Mungu asema "Nitawajaribu katika tanuu ya taabu" (Isaya 48:10) Pamoja na majaribu hayo hatuachi tushindwe kwa kuwa yeye yupo nasi na gongo lake na fimbo yake vyatufariji (Zab 23: 4). Yeye atailinda mienendo yetu na kuhifadhi njia zetu sisi tulio waaminifu wake. (Methali 2:8) na atazinyoosha njia zetu (Yoh. 14:8)

**(b) Majaribu mengine ni kutoka kwa shetani**

- Shetani anamjaribu Ayubu ili amkane Mungu (Ayubu 1:6-22) Ayubu hakufanya dhambi wala kumwazia Mungu kwa upumbavu. Yesu alijaribiwa (Mt. 4: 1-11)
- Bwana kiti chake kiko mbinguni, macho yake yanaangalia wanadamu, kope zake zinawajaribu "Bwana huwajaribu wenye haki:" Zab 11: 11 4[a] 5[a] ) Yer. 20:12) Hivyo kiongozi anapopitiwa na majaribu usifadhaike, usiogope, usimkasirikie Mungu wala usikose kuwa na subira kwani ukifanya hayo utaonyesha huna imani thabiti.
- Katika Uongozi usilewe majivuno, bali uwe mvumilivu katika majaribu, kwani hayo yatakutegemeza upate kuwa mkamilifu na mwaminifu na hautapungukiwa na chochote. (Yak. 1:2 - 4|) kwa maana Mungu huwapa nguvu wale walio waaminifu na uvumilivu. (Nya. 16 : 9) Mkabidhi Bwana njia zako pia umtumaini yeye naye atafanya. (Zab. 37:5)

Mtume Paulo anakiri "mambo haya makuu niliyofunuliwa yasinifanye nilewe majivuno nilipewa maumivu mwilini kama miiba na shetani mwenye kunipiga. Sikustahili kujivuna lakini nilimsihi Bwana jambo hili linitoke. Bwana akaniambia "NEEMA YANGU INATOSHA" Ndipo nikasema "Nakubali kwa radhi udhaifu, dharau, taabu , udhalimu na mateso kwa ajili ya Kristo"(2Kor 12:7 -10)

Hivyo viongozi Walei yatupasa kuyakubali majaribu na mateso kwa ajili ya Ujenzi na Utekelezaji wa Utume wa Walei katika Kanisa, Tuwajibike na kushirikiana katika Kristo.

## MIKUTANO MIKUU/MAALUM

### 1. KAMATI TENDAJI

**Wajumbe**

(a) Kamati Tendaji JNNK
(b) Wenyeviti wa Vyama Mashirika ya Kitume
(c) Makatibu wa Kamati ndogo ndogo

**Majukumu**

(i) Kupokea taarifa na maelekezo kutoka ngazi ya juu na kuyatekeleza
(ii) Kutoa maoni na mapendekezo kwa ngazi ya juu kwa kutumia vyombo husika.
(iii) Kupokea na kupitisha taarifa ya fedha, bajeti, mapato na matumizi
(iv) Kuandaa mkutano wa Halmashauri ya Utekelezaji/ Mikuu

### 2. HALMASHAURI YA UTEKEKELEZAJI

**Wajumbe:**

(a) Wenyeviti JNNK, *JNNK/KIJIJI/MTAA/KANDA/ KIGANGO/PAROKIA NA JIMBO*
(b) Wenyeviti wa vyama na mashirika ya kitume ngazi husika, Makatibu wa Kamati ndogo ndogo

**Majukumu:**

(i) Kupokea taarifa na maelekezo kutoka kamati tendaji ngazi husika na Kanisa
(ii) Kupokea na kupitisha taarifa ya fedha kwa matumizi
(iii) Kufuatilia utekelezaji wa yaliyoandaliwa na kamati tendaji ngazi husika
(iv) Kuandaa Mikutano Mikuu / Maalum

## MIKUTANO MIKUU/MAALUM

### 3. KAMATI TENDAJI

**Wajumbe**

(a) Wenyeviti, Makatibu na Watunza Hazina Vigango, Parokia na Jimbo
(b) Wenyeviti VMJ Kitume ngazi husika
(c) Makatibu wa kamati ndogo ndogo

**Majukumu:**

(i) Kupokea taarifa na maelekezo kutoka ngazi ya JNNK, Jimbo na ya Kanisa
(ii) Kupokea taarifa ya fedha, bajeti, Mapato na Matumizi
(iii) Kufuatilia utekelezaji wa yaliyoazimiwa na vikao/ Mikutano ya Kanisa
(iv) Kuchagua viongozi wapya ngazi husika toka JNNK hadi jimbo

### 4. WAHUSIKA

(a) Kamati tendaji, Baba, familia au mwakilishi
- Wenyeviti wa Vyama na Mashirika ya Kitume
- Makatibu wa Kamati ndogo ndogo

Hawa wanaunda Halmashauri ya utekelezaji JNNK

(b) - Kamati Tendaji, Wenyeviti wa Kijiji/Mtaa/Kanda na Kigango
- Wenyeviti wa vyama Mashirika ya Kitume
- Makatibu wa Kamati ndogo ndogo

Hawa wanaunda Halmashauri ya utekelezaji Kijiji/ Mtaa/Kanda na Kigango

(c) - Kamati Tendaji Wenyeviti Kijiji/ Mtaa na Kigango
- Wenyeviti wa Vyama, Mashirika ya Kitume
- Makatibu wa kamati ndogo ndogo
- Paroko / Wakili Paroko

Hawa wanaunda Halmashauri ya Utekelezaji Parokia

(d) - Kamati Tendaji Wenyeviti Parokia/Vigango Teule
- Wenyeviti wa Vyama/ Mashirika ya Kitume
- Makatibu wa kamati ndogo ndogo\
- Afisa Mtendaji, Mkurugenzi Idara ya Utume wa Walei. Hawa wanaunda Halmashauri ya Utekelezaji jimbo

(e) - Kamati Tendaji, Wenyeviti, Makatibu, Watunza hazina
- Wenyeviti wa Vyama na Masharika
- Paroko/Wakili Paroko - Ngazi ya Kigango na Parokia
- Afisa Mtendaji / Mkurugenzi Idara ya utume wa Walei Ngazi ya jimbo
- Hawa wanashiriki mikutano mikuu ngazi husika.

## 5. JEDWALI VIKAO/MIKUTANO

| S/NO | VIKAO/ MIKUTANO | KAMATI TENDAJI | HALMASHAURI UTEKELEZAJI | MKUTANO MKUU |
|---|---|---|---|---|
| 1. | JNN Kristo Wanajumuiya | Kila wiki kwa sala na majadiliano | Sala | 2 |
| 2. | JNN, MTAA KIGANGO NA PAROKIA | 12 Kila mwezi | Kwa mwaka 3 | 1 |
| 3. | JIMBO | 12 Kila mwezi | Kwa mwaka 3 | 1 |

## 6. TAARIFA ZA VIKAO/MIKUTANO

1. Kamati Tendaji siku saba (7) kabla ya siku ya mkutano
2. Halmashauri ya Utekelezaji siku kumi na nne (14) hadi ishirini na moja (21) kabla ya siku ya mkutano.
3. Mikutano mikuu siku thelathini 30 kabla ya siku ya mikutano

7. **KUHALALISHA KIKAO/MKUTANO**

Idadi ikifikia nusu ya wajumbe wa mkutano ni halali

8. **HITIMISHO**

Ndugu viongozi mikutano ni muhimu sana katika utendaji wetu sisi Walei. Kutokuwepo mikutano kunadhoofisha utume wa Walei kwani kutakosekana uwajibikaji na ushirikiano. Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu, kidole kimoja hakivunji chawa. Ushirikiano huvunja mlima hata kama ungekuwa mgumu kiasi gani. Katika mikutano tunashirikishana ujuzi, elimu, mang'amuzi na namna ya utendaji na ubunifu. Basi tushiriki mikutano kwa kuleta mafanikio yetu Walei na Kanisa zima.

**REJEA**


- Mtaguso mkuu Vatikani II
- Biblia
- Uongozo bora na Padre General Chilambo,
- Katekisimu ya Kanisa Katoliki